

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Telegram “AFYA”, DODOMA  
Namabari ya Simu: +255 026 – 2323267



Mji wa Serikali Mtumba  
Barabara ya Afya

**Barua zote zitume kwa (Katibu Mkuu)**

S.L.P. 743,  
**40478 DODOMA.**  
4 Februari, 2020

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

**Taasisi ya Benjamin William Mkapa imekasimiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto** kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Mifumo Stahimilivu na Endelevu ya Afya (RSSH) kupitia ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund).

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za afya ngazi za vituo katika mikoa kumi (10) iliyopewa kipaumbele na mradi huu ambayo ni; Mwanza, Shinyanga, Mara, Simiyu, Geita, Kagera, Katavi, Tabora, Dodoma na Kigoma.

Taasisi ya Mkapa inapenda **kutangaza nafasi wazi 80 za wataalamu wa afya.** Nafasi hizi ni kwa ajili ya wataalamu waliosomea fani za: -

1. Afisa Muuguzi Msaidizi (Nafasi 30)
2. Muuguzi (Nafasi 40)
3. Mteknolojia Maabara (Nafasi 10)

**Sifa za waombaji;**

1. Waliohitimu mafunzo kutoka katika vyuo vinavyotambulika na Serikali.
2. Wataalamu wenye vyeti kamili vya mafunzo ya fani walizosomea.
3. Wataalamu wenye leseni hai kutoka katika mamlaka za usajili kwa fani zinazotakiwa kufanya usajili kabla ya kuanza kufanya kazi.
4. Mtanzania mwenye umri chini ya miaka 45.
5. Wataalamu ambao wameajiriwa katika ajira za serikali na za mashirika ya dini (Hospitali Teule), hawataruhusiwa kuomba ajira hizi.

**Maombi yote yaambatanishwe na:**

1. Barua ya maombi ya kazi.
2. Nakala ya cheti cha Taaluma.
3. Cheti cha kidato cha nne na sita kama kipo.

4. Picha moja (Passport size)
5. Maelezo binafsi (CV), ikionyesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/ namba ya kiganjani ya wadhamini wa mwombaji ( wasiopungua wawili);
6. Nakala zote za vyeti ziwe zimepitishwa na mwanasheria ili kuthibitisha kama ni nakala halisi ya cheti cha mwombaji.

**Zingatia:**

- **Maombi yote yatumwe kwa njia ya mtandao (online)** kupitia mfumo wa kielektroniki unaopatikana kupitia anuani ya [ajira.moh.go.tz](http://ajira.moh.go.tz)
- **Maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja Ofisini,hayatafanyiwa kazi.**
- Majibu yatatolewa kwa watakaofanikiwa tu.

Tangazo hili la kazi linapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto [www.moh.go.tz](http://www.moh.go.tz) na Taasisi ya Benjamin Mkapa: [www.mkapafoundation.or.tz](http://www.mkapafoundation.or.tz)

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19 Februari, 2020.**

**Imetolewa na;**

**KATIBU MKUU**

**Wizara ya Afya, Maendelo ya Jamii**

**Jinsia, Wazee na Watoto - Afya**